

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOZA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)

Barua Pepe: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOZA**

**3 Barabara ya Rashidi**

**Kawawa,**

S.L.P 5429,

**12880 -DAR ES SALAAM.**

**Tanzania**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**WALEMAVU WALIOKIMBILIA KWA RC MAKONDA SASA WAANZA KUPATA NEEMA.**

Hospitali ya CCBRT imeguswa na kampeni ya Mkuu wa Mkoza wa Dar es Salaam Mheshimiwa PAUL MAKONDA ya kutafuta Miguu Bandia kwa watu wenye uhitaji kwa kuwapatia matibabu Wagonjwa 35 waliokatwa Miguu kutokana na Ugonjwa wa kisukari.

Miguu hiyo ya kisasa ina thamani ya zaidi ya Shilling Million 157 ambapo kati ya Wagonjwa 35 waliokuwa wakitembelea Magongo kwa muda mrefu baada ya kukatwa miguu, 21 wameshawekewa Miguu bandia na sasa wanaendelea na Shuguli zao baada ya kuwa wazima.

RC MAKONDA amesema lengo la kampeni hiyo ni kusaidia wanaotumia Magongo kupata Miguu ya Bandia ya kisasa ili waweze kuendelea na shughuli zao za ujenzi wa Taifa na kuhudumia Familia.

Ameishukuru Hospital ya CCBRT kwa kuunga mkono kampeni hiyo pamoja E FM RADIO na TV E waliooitolea kuhamasisha jamii kuchangia Miguu Bandia.

Katika hatua nyingine RC MAKONDA amepatiwa kiasi cha Shillingi Millions 10,000,000 kutoka kampuni ya Ujenzi ya SPECTUM DESIGN ambapo Mkurugenzi wake Arch.JIMMY MKENDA amesema lengo la kutoa mchango huo ni baada ya kuguswa na kampeni hiyo inayolenga kuwasaidia waliokata tamaa baada ya kupoteza miguu.

Aidha RC MAKONDA amesema kuwa atazungumza na Taasisi zinazotoa Bima ya Afya ili waongeze kipengele cha Matibabu na kutoa Miguu bandia kwa watu waliopoteza Miguu kwa Ajali au Ugonjwa.

Amehamasisha jamii kuchangia kampeni hiyo kupitia CRDB account namba 0150299713500 au kufika Ofisi za Mkuu wa Mkoa au E-FM Radio kisha kuwasilisha mchango wao.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa wale mavu Hospital ya CCBRT BREND A MSANGI amewaasa Wananchi kuchangia kampeni hiyo huku akieleza kuwa wataendelea kushirikiana na Mkuu wa Mkoa.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhushiano

**OFISI YA MKUU WA MKOA**

**DAR ES SALAAM**

17/11/2017